KANUNI ZA UTEUZI FEB '10:Layout 1 6/2/10 3:59 PM Page 1

KANUNI ZA UTEUZI WA WAGOMBEA WA CCM KUINGIA KATIKA VYOMBO VYA DOLA

Toleo la Februari, 2010

Zimetolewa na:
Halmashauri Kuu ya Taifa ya CCM

Bei Sh.500/=

KANUNI ZA UTEUZI FEB '10:Layout 1 6/2/10 3:59 PM Page 2

KANUNI ZA UTEUZI FEB '10:Layout 1 6/2/10 3:59 PM Page 3

CHAMA CHA MAPINDUZI

KANUNI ZA UTEUZI WA WAGOMBEA WA CCM KUINGIA KATIKA VYOMBO VYA DOLA

TOLEO LA FEBRUARI, 2010

KANUNI ZA UTEUZI FEB '10:Layout 1 6/2/10 3:59 PM Page 4

Madhumuni na lengo Kuu la CCM ni hili:

“Kushinda katika Uchaguzi wa Serikali Kuu na Serikali za Mitaa Tanzania Bara na Zanzibar ili kuunda na kushika Serikali Kuu na Serikali za Mitaa katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Zanzibar.”

(KATIBA YA CCM 1977, TOLEO LA 2010)

KANUNI ZA UTEUZI FEB '10:Layout 1 6/2/10 3:59 PM Page 5

YALIYOMO

Ukurasa

1. UTANGULIZI 1

2. FUNGU LA KWANZA

(I) Masharti ya Uongozi katika Serikali 3
(ii) Sifa za Wagombea 6
(a) Ngazi ya Kitongoji hadi Wawakilishi na Wabunge..... 6
(b) Ngazi ya Rais 7

3. FUNGU LA PILI

(i) Utaratibu wa kuomba Uongozi 10
(ii) Malipo wakati wa kuchukua Fomu 12
(iii) Utaratibu wa Wagombea kujieleza 14
(iv) Uhakiki wa Wanachama kwa ajili ya kupiga Kura za Maoni: 15
(v) Utaratibu wa kusimamia Kura za Maoni .. 17
(vi) Siku ya kupiga kura, Utaratibu wa kupiga kura, Kuhesabu kura na Kutangaza matokeo 19

4. FUNGU LA TATU

(i) Uchujaji na Uteuzi wa Wagombea 22
(ii) Mgao wa Viti Maalum wanawake wa mikoa na makundi maalum 36
(iii) Malalamiko ya Uteuzi wa Wagombea 38

KANUNI ZA UTEUZI FEB '10:Layout 1 6/2/10 3:59 PM Page 6

(iv) Miiko ya shughuli za Uchujaji na Uteuzi wa Wagombea 39

5. FUNGU LA NNE
Masuala muhimu ya kuzingatia wakati wa vikao vya Uchujaji na Uteuzi wa Wagombea .. 42

KANUNI ZA UTEUZI FEB '10:Layout 1 6/2/10 3:59 PM Page 7

UTANGULIZI

(I) CCM ni Chama cha Siasa chenye historia ndefu ya mapambano, na pia chenye uwezo mkubwa wa kuongoza Taifa kutokana na kukubalika kwake na wananchi. Hivyo kina wanachama wengi, kina Katiba, Itikadi ya Siasa, Sera za Uwazi na ukweli, Miongozo mbali mbali, na Ilani zake za Uchaguzi wa Serikali za Mitaa kwa ngazi ya Vitongoji, Mitaa, Vijiji, Madiwani; na ya Uchaguzi wa Serikali Kuu.

(II) Chaguzi hizo zote hufanyika kwa mujibu wa Katiba ya Nchi na Sheria zetu za Uchaguzi. Nafasi za uongozi katika vyombo vya Dola ambazo raia wa Tanzania aliye na sifa zinazohitajika anaweza kuchaguliwa kuzishika, ni hizi zifuatazo:-

(1) Mwenyekiti wa Kitongoji

(2) Mwenyekiti wa Kijiji na Wajumbe wa Halmashauri ya Kijiji;

(3) Mwenyekiti wa Mtaa na Wajumbe wa Kamati ya Mtaa.

(4) Diwani wa Kata (Bara) au Wadi (Zanzibar);

(5) Mjumbe wa Baraza la Wawakilishi (Tanzania Zanzibar);

(6) Mbunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania;

KANUNI ZA UTEUZI FEB '10:Layout 1 6/2/10 3:59 PM Page 8

(7) Rais wa Zanzibar;

(8) Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (na Makamu wa Rais);

(9) Madiwani,Wabunge ,na Wawakilishi wa Viti Maalum vya Wanawake.

(III) Kwa kuzingatia Sheria, Kanuni na Taratibu za uchaguzi katika mfumo wa Vyama vingi vya siasa, Chama Cha Mapinduzi kitateua mgombea mmoja kwa kila nafasi inayoshindaniwa kuingia katika chombo cha Dola kinachohusika. Isipokuwa kwamba kwa zile nafasi za viti maalum vya wanawake, Chama Cha Mapinduzi kitateua idadi ya wagombea inayotakiwa kwa mujibu wa Katiba ya nchi, Katiba ya Zanzibar, na sheria za uchaguzi wa Serikali Kuu na Serikali za Mitaa.

(IV) Kanuni hizi zitakuwa ni mwongozo kwa vikao vya CCM vinavyochuja, na vile vinavyofanya uteuzi wa mwisho wa wanachama wa CCM ambao watajitokeza kuomba kugombea nafasi mbalimbali za uongozi katika vyombo vya Dola.

KANUNI ZA UTEUZI FEB '10:Layout 1 6/2/10 3:59 PM Page 9

FUNGU LA KWANZA

KANUNI ZA JUMLA

MASHARTI YA UONGOZI KATIKA SERIKALI

1. Kila mwanachama wa CCM anayegombea na hatimaye kuchaguliwa kushika nafasi yoyote ya uongozi katika Serikali, anapashwa kukiri kwa dhati kwamba maendeleo halisi ya wananchi yanayosimamiwa na Serikali ya CCM katika kipindi kinachohusika, yatapatikana kwa njia ya utekelezaji uliokamilika wa ILANI za CCM za uchaguzi. Kwa hiyo wajibu wake wa kwanza ni kusimamia utekelezaji wa ILANI hizo katika eneo lake la uongozi kwa nguvu na uwezo wake wote.

2. Kiongozi wa kuchaguliwa mwenye madaraka ya utawala -(kwa mfano Mwenyekiti wa Kitongoji, Mtaa, Kijiji au Mbunge, Mwakilishi hata Rais); ana wajibu wa kuhakikisha kwamba kazi zote za Serikali katika ngazi yake zinafanyika kwa ukamilifu na kwa kufuata Sheria, Kanuni na Taratibu zilizowekwa, ili kuondoa malumbano ya kisiasa, vurugu, majungu, uzembe, wizi, rushwa na ubadhilifu wa mali ya umma, mambo ambayo ni kikwazo kikubwa katika suala zima la utawala bora.

3. Kiongozi wa Serikali ya CCM ambaye pia ni mwakilishi wa wananchi ; kwa mfano: Diwani, Mbunge, Mjumbe wa Baraza la Wawakilishi ; anao wajibu mkubwa wa kuhakikisha kwamba:-

KANUNI ZA UTEUZI FEB '10:Layout 1 6/2/10 3:59 PM Page 10

(i) Anatembelea Jimbo lake la uchaguzi mara kwa mara kukagua utekelezaji wa miradi ya maendeleo ambayo imetengewa fedha ili ajionee mwenyewe na kufanya tathmini ya viwango vya utekelezaji ambavyo vimefikiwa. Lengo hapa ni kuharakisha utekelezaji wa miradi hiyo ili iweze kukamilika katika muda uliopangwa, pamoja na kuzuia au kukomesha utekelezaji hewa wa miradi ya maendeleo.

(ii) Kuwatembelea mara kwa mara wananchi wa eneo lake na kusikiliza kero zao, ili aweze kushiriki kwa ukamilifu katika kuzitatua. Kazi hii sharti ifanyike kwa kipindi chote cha miaka mitano ya Uongozi wake.

(iii) Anakuwa karibu na kushirikiana vizuri na vyombo vyote vya Serikali, inayoongozwa na CCM; pamoja na Taasisi nyingine zinazoshiriki katika kuleta maendeleo ya wananchi katika eneo lake la uongozi.

(iv) Kuwafikishia wananchi wa eneo lake maagizo ya Serikali yanayotolewa mara kwa mara, na kuyafafanua vizuri maagizo hayo katika mikutano ya hadhara au katika vikao vya Kiserikali vinavyohusika. Lengo hapa ni kuhakikisha kwamba kila agizo la Serikali limepokelewa na wananchi na linaeleweka ipasavyo ili waweze kulitekeleza kwa ukamilifu kama raia wema wa Tanzania.

KANUNI ZA UTEUZI FEB '10:Layout 1 6/2/10 3:59 PM Page 11

(v) Anahudhuria na kushiriki kwa ukamilifu katika vikao vyote vya Serikali na CCM vinavyomhusu.

(vi) Anajihusisha kwa vitendo na kwa ukamilifu katika uimarishaji wa Chama Cha Mapinduzi katika ngazi ya uongozi wake.

4. Kamati ya Siasa ya Halmashauri Kuu ya ngazi ya uongozi wa Kiongozi anayehusika, itafuatilia mara kwa mara utekelezaji wa wajibu wake huo na kuujadili katika vikao vyake, na baadaye kutoa taarifa kwa vikao vya Chama vya ngazi za juu.

KANUNI ZA UTEUZI FEB '10:Layout 1 6/2/10 3:59 PM Page 12

SIFA ZA WAGOMBEA

Ngazi ya Kitongoji hadi Wawakilishi/Wabunge:

5. Kila raia wa Tanzania anayejitokeza kugombea nafasi ya uongozi Serikalini kwa tiketi ya CCM (ngazi ya Kitongoji hadi Wawakilishi/Wabunge) sharti awe na sifa za jumla zifuatazo:-

   (i) Awe mwanachama wa CCM asiyetiliwa shaka yoyote katika eneo lake, mwadilifu na anayekubalika na wananchi kwa jumla;

   (ii) Awe na sifa zote zinazotakiwa na Katiba ya Nchi au Sheria au Kanuni inayohusu uongozi anaoutaka;

   (iii) Awe anakubali kwa dhati Imani, Malengo, Madhumuni na Sera za CCM;

   (iv) Awe mstari wa mbele katika kuhudhuria vikao vya Chama vinavyomhusu kwa mujibu wa Katiba ya CCM;

   (v) Awe mkweli, mwaminifu kwa CCM na mwenye tabia na mwenendo safi kwa jumla;

   (vi) Awe mpenda maendeleo, mbunifu, hodari wa kazi na mwenye elimu, uzoefu na upeo mkubwa kuhusu maendeleo ya uchumi na jamii na ujenzi wa taifa kwa jumla.

KANUNI ZA UTEUZI FEB '10:Layout 1 6/2/10 3:59 PM Page 13

Ngazi ya Rais

6. Sifa za mwanachama wa CCM atakayeteuliwa kugomea nafasi ya Rais wa Zanzibar, Rais na Makamu wa Rais wa Jamhuri ya muungano wa Tanzania kwa tiketi ya CCM, zitawekwa rasmi na Halmashauri Kuu ya taifa ya CCM kwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo:-

   (i) Uzito wa nafasi hizo kwa nchi yetu

   (ii) Haja ya kulinda na kuendeleza mshikamano wa wana-CCM ndani ya Chama.

   (iii) Haja na umuhimu wa kupanua demokrasia ndani ya CCM katika kuwapata viongozi wa Kitaifa; na

   (iv) Hali halisi ya ushindani wa kisiasa nchini.

Sifa za msingi zifuatazo zitazingatiwa:-

   (i) Awe na uwezo mkubwa wa kuongoza Taifa kwa kuzingatia uzoefu wake katika uongozi wa shughuli za Serikali, Umma au Taasisi;

   (ii) Awe Mwadilifu, mwenye Hekima na Busara;

   (iii) Awe angalau na kiwango cha Elimu ya Chuo Kikuu au Elimu inayolingana na hiyo;

   (iv) Awe mwenye upeo na uwezo mkubwa wa kudumisha, kuimarisha na kuendeleza Muungano wetu, umoja wetu, Amani na Utulivu wetu na Mshikamano wa Kitaifa;

(v) Awe mtu mwepesi wa kuona mbali, asiyeyumbishwa na mwenye uwezo wa kufanya uamuzi wa busara kuhusu masuala nyeti na muhimu ya Taifa kwa wakati unaofaa;

(vi) Awe na upeo mkubwa na usiotiliwa shaka kuhusu masuala ya Kimataifa, ili aweze kuwa kiungo imara kati ya nchi yetu na Dunia yote kwa jumla;

(vii) Asiwe mtu mwenye hulka ya udikteta au ufashisti, bali awe ni mtu anayeheshimu na kulinda Katiba ya Nchi, Sheria, Utawala Bora, Kanuni na Taratibu za Utawala bora;

(viii) Awe mtetezi wa wanyonge, wa Haki za Binadamu, mzingatiaji makini wa maendeleo ya raia wote na asiwe na tamaa ya kujitafutia umaarufu wake binafsi;

(ix) Awe mstari wa mbele katika kuzifahamu, kuzieleza, kuzitetea na kuzitekeleza Sera za CCM na Ilani ya CCM ya Uchaguzi;

(x) Awe mpenda haki na awe mtu jasiri katika kupambana na dhuluma na maovu yote nchini;

(xi) Asiwe ni mtu ambaye anatumia nafasi yake ya Uongozi kujilimbikizia mali;

(xii) Kwa jumla awe ni mtu anayekubalika na wananchi; na

KANUNI ZA UTEUZI FEB '10:Layout 1 6/2/10 3:59 PM Page 15

(xiii) Awe ni mtu makini katika kuzingatia masuala ya uwajibikaji wa viongozi/watendaji, na asiyevumilia uzembe katika utekelezaji wa majukumu/wajibu waliokabidhiwa ili kuinua nidhamu ya Kazi, Tija na Ufanisi.

7. Wagombea wa ngazi zote sharti wawe ni raia wa Tanzania kwa mujibu wa Sheria ya Uraia ya Mwaka 1995. Kwa Mgombea Urais wa Jamhuri ya Muungano, sharti awe raia kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano. Na mgombea Urais wa Zanzibar, sharti awe raia kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano na pia awe ni Mzanzibari kwa mujibu wa Katiba ya Zanzibar.

KANUNI ZA UTEUZI FEB '10:Layout 1 6/2/10 3:59 PM Page 16

FUNGU LA PILI

UTARATIBU WA KUOMBA UONGOZI

8. Ratiba ya Uchaguzi wa Serikali Kuu, Serikali za Mitaa na uchaguzi Mdogo wowote unaofanyika, itawekwa na chombo cha Dola chenye mamlaka na madaraka ya kusimamia Uchaguzi nchini. Mara baada ya ratiba hiyo kutolewa, Katibu wa CCM wa ngazi inayohusika na uchaguzi huo atawapa fomu za kuomba uongozi wanachama wa CCM watakaojitokeza kugombea nafasi wazi iliyopo/zilizopo katika ngazi yake. Tarehe ya kuchukua na kurudisha fomu itawekwa kwa kuzingatia ratiba ya vikao vya uchujaji na uteuzi wa wagombea ndani ya Chama; pamoja na ratiba ya Tume ya taifa ya Uchaguzi.

9. Kila mwanachama wa CCM atakayechukua fomu atatakiwa kurudisha fomu yake kwa katibu wa CCM wa ngazi inayohusika, na ndani ya muda uliowekwa, vinginevyo fomu yake haitapokelewa.

10. Utaratibu wa kuchukua na kurudisha fomu za wagombea uongozi kwa tiketi ya CCM utakuwa kama ifuatavyo:-

    (i) Wanachama wanaogombea nafasi ya uongozi katika ngazi ya Kitongoji, Mtaa na Kijiji, watachukua na kurudisha fomu kwa Katibu wa CCM wa Tawi lenye nafasi husika ya uongozi.

(ii) Wanachama wanaogombea nafasi ya Diwani wa Kata (Bara) au Wadi (Zanzibar) watachukua na kurudisha fomu kwa Katibu wa CCM wa Kata/Wadi inayohusika.

(iii) Wanachama wanaogombea nafasi ya Ubunge au Ujumbe wa Baraza la Wawakilishi watachukua na kurudisha fomu kwa Katibu wa CCM wa Wilaya inayohusika.

(iv) Kuhusu nafasi za udiwani, ubunge na uwakilishi wa viti maalum vya wanawake hakuna mtu yeyote atakayeruhusiwa kugombea tena nafasi hiyo endapo atakuwa ameshika wadhifa huo kwa vipindi viwili mfululizo. Isipokuwa kwamba kanuni hii haitatumika katika uchaguzi mkuu wa 2010.

(v) Wanachama wanaogombea nafasi ya Udiwani viti maalum vya wanawake watachukua na kurudisha fomu kwa Katibu wa Wilaya wa UWT.

(vi) Wanachama wanaogombea nafasi za viti maalum vya wanawake katika Bunge au katika Baraza la Wawakilishi, watachukua fomu na kuzirudisha kwa Katibu wa Mkoa wa UWT.

(vii) Wanachama wanaogombea nafasi ya Rais wa Zanzibar au Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, watachukua na kurudisha fomu kwa Katibu Mkuu wa CCM.

KANUNI ZA UTEUZI FEB '10:Layout 1 6/2/10 3:59 PM Page 18

MALIPO WAKATI WA KUCHUKUA FOMU

11 (1) Kutakuwa na malipo ya aina mbili zifuatazo, ambayo yatatolewa wakati wa kuchukua fomu na kila mgombea wa nafasi kuanzia za Udiwani, Ubunge na Uwakilishi, hadi nafasi za ngazi ya Taifa.

(a) Aina ya kwanza ni malipo ya kuchangia gharama za uendeshaji na usimamizi wa zoezi la kura za maoni. Viwango vya malipo hayo vitakuwa kama ifuatavyo:-

(i)	Fomu za Udiwani	-	Tshs. 10,000/=
(ii)	Fomu za Ubunge/Uwakilishi	-	Tshs,100,000/=
(iii)	Fomu za Uspika	-	Tshs.500,000/=
(iv)	Fomu za Urais	-	Tshs.1,000,000/=

Mgao wa Mapato hayo utakuwa kama ifuatavyo:-

(i) Kata/Wadi inayohusika itapewa asilimia 100 ya mapato yote yatakayotokana na fomu za Wagombea Udiwani.

(ii) Wilaya inayohusika itapewa asilima 100 ya mapato yote yanayotokana na fomu za wagombea Ubunge/Uwakilishi.

(iii) Mapato yatakayotokana na fomu za wagombea Uspika pamoja na Urais, yatagawanywa kama ifuatavyo:-

a. **Uspika wa Baraza la Wawakilishi:**
Afisi Kuu ya CCM Zanzibar itapewa asilimia 100

b. **Urais wa Zanzibar:**
Afisi Kuu ya CCM Zanzibar itapewa asilimia 100

c. **Uspika wa Bunge:**
Makao Makuu ya CCM yatapewa asilimia 100.

d. **Urais wa Jamhuri ya Muungano:**
Makao Makuu ya CCM yatapewa asilimia 100

(b) Aina ya pili itakuwa ni malipo ya kuchangia gharama za usafiri wa pamoja kwa wagombea wa Udiwani, Ubunge, na Uwakilishi ambao utaandaliwa na Kamati ya Siasa ya Halmashauri Kuu ya Wilaya. Kiwango cha mchango wa kila mgombea kitaamuliwa na Kamati ya Siasa ya Halmashauri Kuu ya Wilaya inayohusika, kwa kuzingatia mazingira ya Wilaya hiyo, hususan ukubwa wa Wilaya, uwingi wa vituo vya wagombea kujieleza vilivyopangwa na Kamati hiyo, na urefu wa masafa ya kwenda na kurudi kutoka kwenye vituo vyote hivyo.

Mgao wa mapato hayo utakuwa kama ifuatavyo:-

a. Wilaya husika itapewa asilimia 100 ya

mapato yote yatakayotokana na fomu za wagombea Ubunge na Uwakilishi.

- Kata/Wadi inayohusika itapewa asilimia 100 ya michango ya Fomu za Wagombea Udiwani.

(2) Gharama nyingine zinazohusu maandalizi ya madaftari mapya ya Wanachama wa CCM kwa ajili ya zoezi la kura za maoni; maandalizi ya mikutano ya Kampeni kwa ajili ya Wagombea kutafuta kura za maoni, pamoja na uendeshaji na usimamizi wa mikutano hiyo; na vile vile gharama za mafunzo maalum kwa Viongozi na Watendaji wa CCM wa ngazi zinazohusika moja kwa moja na uendeshaji wa zoezi hilo; zote zitalipwa na Chama Cha Mapinduzi.

UTARATIBU WA WAGOMBEA KUJIELEZA

12 (1) Wagombea wote ambao wameteuliwa rasmi kwa ajili hiyo watasafirishwa kwa pamoja kwa kutumia usafiri ambao umeandaliwa na Kamati ya Siasa ya Halmashauri Kuu ya Wilaya na Kata/Wadi inayohusika, kwenda na kurudi kutoka kwenye vituo vya wagombea kujieleza vilivyoandaliwa na Kamati hiyo. Anayetaka kutumia usafiri wake mwenyewe ataruhusiwa, lakini atatakiwa kuwa katika msafara ulioandaliwa na Chama.

(2) Katika kupanga ratiba na idadi ya vituo vya Mikutano ya kampeni za kura za maoni, Kamati ya Siasa ya Halmashauri Kuu ya Wilaya na Kata/Wadi

itazingatia umuhimu wa kumalizika kwa kampeni zote ndani ya muda wa kampeni hizo uliowekwa na Halmashauri Kuu ya Taifa. Kwa kuzingatia sharti hilo, vituo vya kampeni vyaweza kuwa ni Tawi la CCM, au Kata/Wadi; au maeneo mengine yanayofaa, kulingana na mazingira ya Wilaya inayohusika.

(3) Kabla ya kuanza kwa ratiba ya mikutano ya kampeni za kujieleza, wagombea wote wa nafasi za udiwani, ubunge au Uwakilishi watatakiwa kuhudhuria kwa pamoja kikao maalum cha kamati ya Siasa ya Halmashauri Kuu ya Wilaya na Kata/Wadi, ambapo watajadili na kuafikiana juu ya ratiba ya mikutano hiyo. Lakini agenda kubwa zaidi ya kikao hicho itakuwa ni kusisitiza umuhimu wa kuzingatia maadili ya Chama na miiko ya uchaguzi wa ndani ya Chama.

UHAKIKI WA WANACHAMA KWA AJILI YA KUPIGA KURA ZA MAONI

13 (1) Katika zoezi la kupiga kura za maoni, kila mwanachama wa CCM ambaye kadi yake mpya au ya zamani ya uwanachama imehakikiwa na uhalali wake kuthibitishwa, atakuwa na haki ya kupiga kura ya maoni kwa wagombea wa nafasi za kuingia kwenye vyombo vya Dola. Kwa ajili hiyo, kutakuwa na hatua mbili za uhakiki wa wanachama. Hatua ya kwanza ni kwa mwanachama kuorodheshwa katika Daftari la wanachama wa CCM lililopo kwenye Tawi lake la CCM. Hatua ya pili ni kwa kadi ya mwanachama kuhakikiwa katika kituo cha kupigia kura za maoni.

KANUNI ZA UTEUZI FEB '10:Layout 1 6/2/10 3:59 PM Page 22

Uhakiki kwa njia ya madaftari ya Wanachama wa CCM

(2) Kutakuwa na madaftari ya wanachama wa CCM katika kila Tawi, ambayo yataandaliwa mapema na Makao Makuu ya CCM kwa ajili ya zoezi la upigaji kura za maoni, yakiwa na sura, muundo na ubora unaofanana kwa nchi nzima. Madaftari hayo yatafungwa ifikapo tarehe 30 Juni ya mwaka wa Uchaguzi Mkuu wa Serikali, ili yaweze kuhakikiwa kabla ya kuanza zoezi la upigaji kura za maoni.

Kwa upande wa chaguzi ndogo, madaftari hayo yatafungwa katika muda utakaoamuliwa na Kamati Kuu ya Halmashauri kuu ya Taifa, kulingana na tarehe ya kuanza kwa zoezi la upigaji kura za maoni katika Jimbo au Kata/Wadi inayohusika.

(3) Namna ya kufunga Daftari la Wanachama kwa madhumuni ya upigaji kura za maoni, itakuwa ni kwa Katibu wa CCM wa kila Tawi kwa usimamizi wa Kamati ya Siasa ya Halmashauri Kuu ya Tawi; kupiga mstari chini ya jina la mwanachama wa mwisho aliyeandikishwa kwenye Daftari hilo tarehe 30 Juni.

Uhakiki katika Vituo vya kupigia kura za maoni

(4) Kila mwanachama atajiandikisha katika tawi moja tu kwa madhumuni ya kupiga kura za

KANUNI ZA UTEUZI FEB '10:Layout 1 6/2/10 3:59 PM Page 23

maoni. Inapofika siku ya kupiga kura za maoni, Kamati ya Siasa ya Halmashauri Kuu ya Tawi itakuwa na jukumu la kuhakiki uhalali wa kadi ya kila mwanachama anayewasili kwenye kituo cha kupigia kura. Ni baada tu ya kadi yake kuwa imehakikiwa, ndipo mwanachama huyo atakapoweza kupewa karatasi ya kupigia kura.

(5) Pamoja na kadi yake ya uanachama wa CCM, mwanachama huyo atatakiwa aonyeshe kadi yake ya kupiga kura iliyotolewa na Tume ya Taifa ya Uchaguzi, ili kuhakikisha kuwa anayosifa ya kupiga kura katika Uchaguzi wa Dola unaohusika, ili aweze kutimiza wajibu wake wa kukipatia Chama cha Mapinduzi ushindi. Aidha, atatakiwa awe ametimiza wajibu wa kulipia ada za uanachama wake hata kama sio ada zote kwa ukamilifu, lakini angalau awe amelipa kiwango fulani cha ada anazodaiwa.

(6) Mwanachama yeyote wa CCM ambaye atatoa au kupokea kadi ya CCM bila kufuata utaratibu uliowekwa katika ibara ya 9 na 10 za katiba ya CCM atakuwa ametenda kosa na ataadhibiwa kwa mujibu wa kanuni za CCM za uongozi na maadili.

UTARATIBU WA KUSIMAMIA KURA ZA MAONI

14 (1) Katika ngazi ya Kitongoji, upigaji kura za maoni utasimamiwa na viongozi watatu walioteuliwa mapema na kuandaliwa vizuri kwa

ajili hiyo na Kamati ya Siasa ya Tawi linalohusika.

(2) Katika ngazi ya Mtaa au Serikali ya Kijiji, kura za maoni zitasimamiwa na viongozi watatu walioteuliwa mapema na kuandaliwa vizuri kwa ajili hiyo na kamati ya Siasa ya Kata/Wadi inayohusika.

Wajumbe wote wa Halmashauri Kuu ya Kata/Wadi watapangwa vizuri na Sekretarieti ya ngazi hiyo ili waratibu kazi hii katika Mitaa yote na Vijiji vyote.

(3) Kwa wagombea wa Udiwani, kazi ya kuratibu zoezi la upigaji wa kura za maoni itafanywa na wajumbe watatu wa Halmashauri Kuu ya Kata/Wadi inayohusika, walioteuliwa mapema na kuandaliwa vizuri kwa madhumuni hayo na Kamati ya Siasa ya Kata/Wadi hiyo, pamoja na Wajumbe wawili wa Halmashauri Kuu ya Jimbo/Wilaya watapangwa na Sekretarieti ya ngazi hiyo, kwenda katika kila Tawi la CCM la Kata/Wadi hiyo, kwa ajili ya kuratibu kazi hii, na kuhakikisha kuwa inafanyika vizuri ipasavyo.

(4) Kwa wagombea wa Ubunge/Uwakilishi, kazi ya kuratibu zoezi la upigaji wa kura za maoni itafanywa na Wajumbe watatu wa Halmashauri Kuu ya Jimbo/Wilaya, walioteuliwa mapema na kuandaliwa vizuri kwa madhumuni hayo na Kamati ya Siasa ya Wilaya pamoja na Wajumbe

wawili wa Halmashauri Kuu ya Mkoa watapangwa na Sekretarieti ya ngazi hiyo kwenda katika kila Jimbo la Uchaguzi la Mkoa huo, kwa ajili ya kuratibu kazi hii, na kuhakikisha kuwa inafanyika vizuri ipasavyo.

(5) Upigaji kura za maoni katika kila Tawi utasimamiwa na wajumbe watatu wa Halmashauri Kuu ya Kata/Wadi wanaotoka Tawi la jirani walioteuliwa mapema na kuandaliwa vizuri na kamati ya siasa ya Kata/Wadi inayohusika kwa ajili ya kazi hiyo.

SIKU YA KUPIGA KURA, UTARATIBU WA KUPIGA KURA, KUZIHESABU KURA NA KUTANGAZA MATOKEO YAKE

15 (1) Siku ya kupiga kura za maoni itakuwa ni moja tu, ambayo ni ile siku inayofuata mara baada ya kipindi cha kampeni za wagombea kujieleza kwa wanachama kitakapokuwa kimemalizika.

(2) Utaratibu wa kupiga kura utakuwa kama ifuatavyo:-

(a) Kura za maoni zitapigiwa kwenye kituo cha kupigia kura katika kila Tawi la CCM.

(b) Muda wa kupiga kura za maoni utakuwa ni kuanzia saa 2.00 asubuhi na kuendelea hadi saa 10.00 jioni. Mwanachama atakayewasili kwenye kituo cha kupigia kura baada ya saa 10.00 kupita, hataruhusiwa kupiga kura. Isipokuwa

kwamba mwanachama yeyote aliyekwisha kufika kwenye kituo chake kabla ya saa 10.00 jioni, na yupo hapo anasubiri tu zamu yake ifike ya kupiga kura, mwanachama huyo atapewa fursa ya kupiga kura yake hata kama ni baada ya saa 10.00 jioni.

(3) Utaratibu wa kuhesabu na kutangaza kura utakuwa kama ifuatavyo:-

(a) Kura za maoni zitahesabiwa kwenye vituo vya kupigia kura, na matokeo yake yatatangazwa na kiongozi wa Wasimamizi wa upigaji kura hapo hapo katika kituo kinachohusika. Taarifa ya matokeo hayo itabandikwa mahali pa wazi nje ya kituo hicho, na nakala yake kuwasilishwa haraka iwezekanavyo kwa Katibu wa CCM wa Wilaya inayohusika, kwa ajili ya zoezi la kujumlisha kura zote zilizopigwa kwa kila nafasi.

(b) Kila mgombea, au wakala wake, atapewa fursa ya kushuhudia zoezi hilo la kuhesabu kura. Baada ya zoezi hilo kukamilika, wafuatao watatakiwa kuweka saini zao katika fomu za matokeo ya kura hizo, kama uthibitisho wa usahihi wake:-

(i) Wasimamizi wa kura za maoni.

KANUNI ZA UTEUZI FEB '10:Layout 1 6/2/10 3:59 PM Page 27

(ii) Katibu wa CCM wa Tawi linalohusika.
(iii) Mgombea au wakala wake.

(c) Baada ya kupokea matokeo ya kura za maoni kutoka katika Matawi yote, Katibu wa CCM wa Wilaya, chini ya usimamizi wa Kamati ya Siasa ya Wilaya yake, atazijumlisha kura hizo ili kupata idadi ya kura za maoni alizopata kila mgombea, na kutangaza rasmi hadharani matokeo hayo.

(d) Mara baada ya matokeo kutangazwa, au mapema iwezekanavyo baada ya hapo, wagombea wote waliopigiwa kura za maoni watatakiwa kuhudhuria kikao maalum cha Kamati ya Siasa ya Wilaya, ambacho agenda yake kuu itakuwa ni kuvunja makundi ya wagombea husika, ili kuimarisha umoja na mshikamano ndani ya Chama kwa madhumuni ya kukipatia Chama ushindi katika uchaguzi wa Dola unaofuata.

KANUNI ZA UTEUZI FEB '10:Layout 1 6/2/10 3:59 PM Page 28

FUNGU LA TATU

UCHUJAJI NA UTEUZI WA WAGOMBEA

16. (1). Mgombea yeyote wa CCM anayetaka kuingia katika chombo cha Dola, atateuliwa kwa kuzingatia kura za maoni zilizopigwa. Mgombea atakayeteuliwa ni yule anayeongoza kwa wingi wa kura za maoni alizopata. Isipokuwa kwamba endapo itathibitika kuwa kura hizo za ushindi alizipata kwa njia ya rushwa, kikao cha uteuzi wa mwisho hakitamteua kugombea nafasi anayoiomba.

(2) Endapo, kwa sababu maalum, Kamati Kuu ya Halmashauri Kuu ya Taifa itaona kuwa hakuna haja ya kuitisha kura za maoni, hususan katika uchaguzi mdogo, itakuwa na uwezo wa kuelekeza kwamba zoezi la kura za maoni lisifanyike.

17. Utaratibu wa kuchuja na hatimaye kuteua mgombea/wagombea wa kila ngazi utakuwa kama ifuatavyo:-

(i) **Ngazi ya Kitongoji:**

(1) Wagombea watapigiwa kura za maoni na mkutano wa Wanachama wote wa Shina. Sharti la Akidi halitatumika katika mkutano wa kupiga kura za maoni.

(2) Kamati ya Siasa ya Tawi ambamo Shina/Mashina yamo itawajadili wagombea wote.

(3) Halmashauri Kuu ya CCM ya Kata/Wadi itafanya uteuzi wa mwisho wa mwanachama wa CCM atakayesimama kugombea nafasi wazi ya Mwenyekiti wa Kitongoji kinachohusika.

(ii) **Ngazi ya Kijiji na Mtaa**

(1) Wagombea wote watapigiwa kura za maoni na Mkutano wa wanachama wote. Sharti la Akidi halitatumika katika mkutano wa kupiga kura za maoni wa CCM wa Tawi.

(2) Kamati za Siasa za Halmashauri Kuu za Matawi na Kata/Wadi zinazohusika zitawajadili wagombea.

(3) Halmashauri Kuu ya CCM ya Wilaya itafikiria na kufanya uteuzi wa mwisho wa wanachama watakaosimama kugombea Uenyekiti wa Mtaa, Ujumbe wa Kamati ya Mtaa, Uenyekiti wa Kijiji na Ujumbe wa Halmashauri ya Kijiji.

(iii) **Diwani wa Kata au Wadi:**

(1) Wagombea watapigiwa kura za maoni na wanachama wote wa CCM wa Kata au Wadi inayohusika wakiwa katika matawi

KANUNI ZA UTEUZI FEB '10:Layout 1 6/2/10 3:59 PM Page 30

yao ya CCM, ambao wamehakikiwa kwa mujibu wa Kanuni ya 13(1) ya kanuni hizi, na kwa kufuata utaratibu ulioelezwa katika Kanuni ya 16 ya Kanuni hizi.

(2) Kamati ya Siasa ya Halmashauri Kuu ya CCM ya Tawi linalohusika itawajadili wagombea.

(3) Kamati za Siasa za Kata/Wadi, Jimbo, Wilaya na Mkoa zitawajadili wagombea na kuwatolea mapendekezo yao.

(4) Halmashauri Kuu ya CCM ya Mkoa itafikiria na kufanya uteuzi wa mwisho wa mwanachama mmoja atakayesimama kugombea nafasi ya Diwani katika kila Kata au Wadi ambayo imo katika Mkoa unaohusika. Katika kufanya kazi hiyo kwa upande wa madiwani wanaomaliza muda wao, Halmashauri Kuu ya CCM ya Mkoa itazingatia pia tathmini iliyofanywa ya utendaji kazi wao katika kipindi kinachomalizika.

(iv) **Ngazi ya Diwani - Viti Maalum Wanawake:**

(1) Wagombea watapigiwa kura za maoni na Mkutano Mkuu wa UWT Wilaya.

(2) Kamati ya Siasa ya Halmashauri Kuu ya CCM ya Wilaya itawajadili wagombea na

kuandaa orodha ya majina kwa kuzingatia idadi inayotakiwa kwa mujibu wa Sheria ya Uchaguzi.

(3) Halmashauri Kuu ya Mkoa itafikiria na kufanya uteuzi wa mwisho wa wagombea udiwani wa viti maalum waliojitokeza katika mkoa huo.

(4) Tume ya Uchaguzi itazingatia na kutangaza washindi ambao watakuwa sawa na asilimia 40 ya Madiwani wote wa Kata au Wadi katika Mamlaka ya Serikali za Mitaa inayohusika.

(v) **Ngazi ya Baraza la Wawakilishi/Bunge:**

(1) Wagombea watapigiwa kura za maoni na wanachama wote wa CCM waliohakikiwa kwa mujibu wa Kanuni ya 13(1) ya Kanuni hizi wakiwa katika Matawi yao ya CCM, na kwa kufuata utaratibu ulioelezwa katika Kanuni ya 16 ya Kanuni hizi.

(2) Kamati ya Siasa ya Halmashauri Kuu ya Wilaya itawajadili wagombea, na kutoa mapendekezo yake kwa Kamati ya Siasa ya Halmashauri Kuu ya Mkoa.

(3) Kwa upande wa Tanzania Bara, Kamati ya Siasa ya Halmashauri Kuu ya CCM ya

Mkoa itawajadili wagombea na kuwatolea mapendekezo yake kwa Kamati Kuu ya Halmashauri Kuu ya Taifa. Kwa upande wa Tanzania Zanzibar, Kamati ya Siasa ya Mkoa itawajadili wagombea na kuwatolea mapendekezo yake kwa Kamati Maalum ya Halmashauri Kuu ya CCM ya Taifa Zanzibar ambayo nayo itatoa mapendekezo yake kwa Kamati Kuu ya Halmashauri Kuu ya Taifa ya CCM .

(4) Kamati Kuu itawajadili wagombea wote na kutoa mapendekezo yake kwa Halmashauri Kuu ya CCM ya Taifa kwa ajili ya uteuzi wa mwisho.

Katika kufanya kazi hiyo kwa upande wa Wabunge/Wawakilishi wanaomaliza muda wao, Kamati Kuu itazingatia pia tathmini itakayokuwa imefanyika ya utendaji kazi wao katika kipindi kinachomalizika.

(vi) **Ngazi ya Uwakilishi/Ubunge - Viti Maalum Wanawake:**

(1) Wagombea waliorudisha fomu zao kwa katibu wa UWT wa mkoa husika watapigiwa kura za maoni na Mkutano Mkuu wa UWT wa Mkoa huo, isipokuwa wagombea wa kundi la VIJANA ambo

KANUNI ZA UTEUZI FEB '10:Layout 1 6/2/10 3:59 PM Page 33

watapigiwa kura na Mkutano Mkuu wa UVCCM Mkoa, kwa kuzingatia utaratibu ufuatao;-

(a) **Kundi la wote la wagombea Ubunge**
Majina matano ya kwanza yaliyoongoza kwa wingi wa kura katika kundi hilo la wote la wagombea ubunge

(b) **Makundi maalum ya wagombea Ubunge**
Jina mojamoja lililoongoza kwa wingi wa kula katika kila kundi la WASOMI; WALEMAVU; WAFANYAKAZI na NGOs zinazotambuliwa kisheria ambazo zinashughulikia mahsusi masuala ya wanawake.

(c) **Kundi la wote la wagombea Uwakilishi**
Majina matatu ya kwanza yaliyoongoza kwa wingi wa kura katika kundi hili la wote la wagombea ujumbe wa Baraza la Wawakilishi.

(d) **Makundi maalum ya wagombea Uwakilishi**
Majina matatu ya kwanza yaliyoongoza kwa wingi wa kura katika kila kundi la WASOMI na WALEMAVU.

(2) Kamati za Siasa za Mikoa ya Tanzania Bara zitawajadili wagombea hao na

kuwasilisha maoni/mapendekezo yao kwa Baraza Kuu la UWT Taifa. Kwa upande wa Tanzania Zanzibar, maoni na mapendekezo ya kamati za Siasa za Mikoa yatawasilishwa kwa Kamati Maalum ya Halmashauri Kuu ya Taifa, ili yakajadiliwe kabla ya kuwasilishwa kwenye Baraza Kuu la UWT Taifa.

(3) (a) Kwa upande wa wagombea Ubunge Baraza kuu la UWT Taifa litawajadili wagombea wa kundi la wote na kupendekeza majina matatu ya wagombea ubunge wa kila mkoa. Aidha, Baraza Kuu litawajadili wagombea ubunge wa yale makundi maalum na kupendekeza idadi ya wagombea wa kila kundi inayotakiwa kwa mujibu wakanuni hizi; yaani VIJANA (10); WASOMI (3); WALEMAVU (3); WAFANYAKAZI (2); NGOs zinazohusika (2); na VIONGOZI WAKUU WA UWT (2).

(b) Kwa upande wa wagombea Ujumbe wa Baraza la Wawakilishi, Baraza Kuu litawajadili wagombea wa kundi la wote na kupendekeza majina mawili ya wagombea uwakilishi kwa kila mkoa. Aidha, Baraza Kuu litawajadili wagombea wa yale makundi maalum, na kupendekeza idadi inayotakiwa kwa kila kundi kwa mujibu wa kanuni hizi; ambayo ni VIJANA (5);

KANUNI ZA UTEUZI FEB '10:Layout 1 6/2/10 3:59 PM Page 35

WASOMI (2); WALEMAVU (2) na KIONGOZI MKUU WA UWT ZANZIBAR (1).

(c) Baraza Kuu la UVCCM ndilo litakalo chagua idadi ya Vijana inayotakiwa na kuwasilisha matokeo hayo kwa Baraza Kuu la UWT.

(d) Baada ya hapo, Baraza Kuu litaandaa orodha zifuatazo ambazo zitawasilishwa kwa Halmashauri Kuu ya CCM Taifa;-

(i) Orodha ya wagombea nafasi 100 (mia moja) za wabunge kwa mgawanyo wa wagombea 78 katika kundi la wote;- yaani wagombea watatu kutoka kila mkoa; wagombea 20 wa makundi maalum na wagombea 2 ambao ni viongozi wakuu wa UWT.

(ii) Orodha ya wagombea nafasi 20 za Ujumbe wa Baraza la Wawakilishi, kwa mgawanyo wa wagombea 10 katika kundi la wote; yaani wagombea wawili kwa kila mkoa; wagombea 9 wa makundi maalum; na mgombea mmoja ambaye ni kiongozi mkuu wa UWT Zanzibar.

(iii) Katika kuandaa orodha hizo zote Baraza Kuu litazingatia sifa za wagombea, umuhimu wa kuwa na mgombea au

KANUNI ZA UTEUZI FEB '10:Layout 1 6/2/10 3:59 PM Page 36

wagombea kutoka katika kila Mkoa na pia kutoka kila kundi miongoni mwa yale makundi maalum; na kwa upande wa wagombea Ubunge, kuweka uwiano unaostahiki baina ya Tanzania Bara na Zanzibar.

(vii) **Rais wa Zanzibar**

(1) Isipokuwa kama Kamati Kuu itaelekeza vinginevyo kila mgombea anatakiwa apate wadhamini 250 kutoka Mikoa isiyopungua mitatu ikiwemo angalau mkoa mmoja kutoka Pemba na mmoja kutoka Unguja. Mjumbe yeyote wa Halmashauri Kuu ya Taifa na Mjumbe mwingine yeyote wa Mkutano Mkuu wa Taifa hataruhusiwa kumdhamini mgombea Urais wa Zanzibar.

(2) Kamati Maalum ya Halmashauri Kuu ya Taifa itawachuja wagombea wote waliojitokeza na kutoa mapendekezo yake ya majina yasiyozidi matano kwa Kamati Kuu ya Halmashauri Kuu ya Taifa, bila ya kuyapigia kura.

(3) Kamati Kuu ya Halmashauri Kuu ya Taifa itapitia sifa za Wagombea hao na kutoa mapendekezo yake ya majina yasiyozidi matatu kwa Halmashauri Kuu ya Taifa kwa ajili ya uteuzi wa mwisho. Isipokuwa kwamba endapo Kamati Kuu itapendekeza jina moja tu, Halmashauri

Kuu ya Taifa itapiga kura za “Ndiyo” au “Hapana”

(4) Halmashauri Kuu ya Taifa itapiga kura za siri kuchagua jina moja la mwanachama wa CCM atakayesimama katika uchaguzi wa Rais wa Zanzibar kwa tiketi ya CCM.

(viii) **Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania:**

(1) Isipokuwa kama Kamati Kuu itaelekeza vinginevyo, kila mgombea wa nafasi hii anatakiwa apate Wadhamini 250 kutoka mikoa isiyopungua 10, angalau miwili kati ya hiyo itoke Tanzania Zanzibar. Mjumbe yeyote wa Halmashauri Kuu ya Taifa na Mjumbe mwingine yeyote wa Mkutano Mkuu wa Taifa hataruhusiwa kumdhamini mgombea Urais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

(2) Kamati Kuu ya Halmashauri Kuu ya Taifa itapitia sifa za wagombea wote na kutoa mapendekezo yake ya majina yasiyozidi matano kwa Halmashauri Kuu ya Taifa.

(3) Halmashauri Kuu ya Taifa itafikiria na kupiga kura za siri ili kupendekeza majina yasiyozidi matatu kwa Mkutano Mkuu wa CCM wa Taifa, kwa ajili ya uteuzi wa mwisho.

Isipokuwa kwamba endapo Halmashauri

Kuu ya Taifa itapendekeza jina moja tu, Mkutano Mkuu wa Taifa utapiga kura za “Ndiyo” au “Hapana”

(4) Mkutano Mkuu wa Taifa utawapigia kura wagombea hao ili kuchagua jina moja la mwanachama wa CCM atakayesimama katika uchaguzi wa Rais wa Jamhuri ya Muungano. Mshindi atakuwa ni yule aliyepata zaidi ya asilimia 50 ya kura halali zilizopigwa.

(5) Zoezi zima la uteuzi wa mgombea wa nafasi hii litafanyika na kukamilika angalau miezi sita kabla ya siku ya Uchaguzi wenyewe iliyowekwa na Tume ya Taifa ya Uchaguzi kuhusu uchaguzi wa Rais wa Jamhuri ya Muungano.

(ix) **Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania**

(1) Huyu atakuwa mgombea mwenza wa mwanachama wa CCM aliyechaguliwa na Mkutano Mkuu wa Taifa kusimama katika uchaguzi wa Rais wa Jamhuri ya Muungano.

(2) Utaratibu wa kumpata mgombea Mwenza utakuwa kama ifuatavyo:-

(i) Mgombea wa Urais wa Jamhuri ya Muungano akitoka upande mmoja wa Jamhuri, Makamu wake atatoka upande wa pili wa Jamhuri ya Muungano.

(ii) Baada ya kumpata mgombea wa CCM wa nafasi ya Rais wa Jamhuri ya Muungano, mgombea huyo atashauriana na Kamati Kuu juu ya mwana-CCM anayemfikiria awe Mgombea Mwenza (Makamu wa Rais).

(iii) Mgombea Urais atatamka jina la mgombea mwenza mbele ya Mkutano Mkuu wa Taifa.

(iv) Mgombea Urais akichaguliwa na wananchi kuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano, mgombea mwenza atakuwa Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano.

(3) Endapo nafasi ya Makamu wa Rais itakuwa wazi wakati wowote, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania atashauriana na Kamati Kuu juu ya mwana- CCM anayefikiria kumteua awe Makamu wa Rais.

(x) **Spika**

(1) Wanachama wanaoomba nafasi ya Uspika wa Bunge/Baraza la Wawakilishi watajadiliwa na Kamati Kuu ya Halmashauri Kuu ya Taifa. Kwa upande wa Tanzania Zanzibar, Kamati Maalum

ya Halmashauri Kuu ya Taifa itawajadili na kutoa mapendekezo yake kwa Kamati Kuu. Kamati Kuu itawachuja waombaji wote na kuteua majina yasiyozidi matatu ya wagombea wa kila moja ya nafasi hizo.

(2) Kamati ya Wabunge/Wawakilishi wote wa CCM itachagua jina moja la mgombea wa CCM wa kila nafasi na kuliwasilisha kunakohusika.

(xi) **Meya na Naibu Meya wa Jiji**

Kamati ya Siasa ya Mkoa itawajadili wanaogombea nafasi za Meya na Naibu Meya wa Jiji au Mji wenye hadhi ya Jiji na kutoa mapendekezo yake kama ifuatavyo:-

(1) Kamati ya Siasa ya Mkoa itajadili na kuteua majina yasiyozidi matatu ya wagombea nafasi ya Naibu Meya wa Jiji na kuyawasilisha kwa Kamati ya Madiwani wote wa CCM katika Jiji linalohusika.

(2) Kwa upande wa Tanzania Bara itapendekeza majina ya wanaogombea Umeya wa Jiji na Manispaa na kuwasilisha majina hayo kwa Kamati Kuu kwa uteuzi wa mwisho. Kwa upande wa Tanzania Zanzibar, majina hayo yaliyopendekezwa yatawasilishwa kwanza kwa Kamati Maalum ya Halmashauri Kuu ya Taifa kabla ya kupelekwa kwa Kamati Kuu. Kamati Kuu itateua majina matatu yatakayowasilishwa kwa Kamati ya Madiwani wote wa CCM katika jiji/Manispaa inayohusika.

(3) Kamati ya Madiwani wote wa CCM wa Jiji itachagua jina moja la mgombea wa CCM wa kila nafasi na kuliwakilisha kunakohusika.

(xii) **Naibu Meya wa Manispaa, Mwenyekiti na Makamu Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya/Mji na Wilaya**

(1) Kamati ya Siasa ya Wilaya itawajadili wagombea wa nafasi hizi na kuwasilisha mapendekezo yake kwa Kamati ya Siasa ya Mkoa.

(2) Kamati ya Siasa ya Mkoa itateua majina yasiyozidi matatu kwa kila nafasi na kuyawasilisha kwa Kamati ya Madiwani wote wa CCM wa Manispaa au Halmashauri ya Wilaya/Mji inayohusika.

(3) Kamati ya Madiwani wote wa CCM wa Manispaa au Halmashauri ya Wilaya/Mji itachagua jina moja la mgombea wa CCM wa kila nafasi inayohusika na kuliwasilisha kunakohusika.

(xiii) **Uteuzi wa mwisho wa wagombea**

Katika vikao vya mwisho vinavyofanya uchaguzi wa kumpata mgombea mmoja ambaye Chama Cha Mapinduzi kitawasilisha jina lake katika vyombo vya Dola, ni yule atakayekuwa amepata zaidi ya nusu ya kura zote halali zilizopigwa.

KANUNI ZA UTEUZI FEB '10:Layout 1 6/2/10 3:59 PM Page 42

MGAO WA VITI MAALUMU WANAWAKE KWA MIKOA NA MAKUNDI MAALUM

18 (1) Baraza Kuu la UWT Taifa litawajadili wagombea wote waliopigiwa kura za maoni, na kuandaa orodha moja itakayowasilishwa kwenye Halmashauri Kuu ya Taifa ya CCM. Katika kuandaa orodha hiyo, Baraza Kuu la UWT Taifa litazingatia umuhimu wa kuwa na wagombea kutoka kila Mkoa; na vile vile kutoka kila kundi la makundi ya VIJANA, WASOMI, WALEMAVU, WAFANYAKAZI, na NGOs.

(2) Kutakuwa na jumla ya nafasi 100 katika Bunge la Jamhuri ya Muungano, ambazo zitagombewa na Mikoa yote pamoja na Makundi hayo yaliyotajwa, pamoja na kundi lingine la Viongozi Wakuu wa UWT ngazi ya Taifa. Nafasi hizo zimegawanywa na Halmashauri Kuu ya Taifa kama ifuatavyo:-

(a) MIKOA YOTE:
Nafasi 3 kwa kila Mkoa, kwa mikao 26.
Jumla ya nafasi za Mikoa ni 78.

(b) MAKUNDI:

(i)	Viongozi Wakuu wa UWT - Nafasi	2
(ii)	NGOs - Nafasi	2
(iii)	WAFANYAKAZI - Nafasi	2
(iv)	WALEMAVU - Nafasi	3
(v)	WASOMI - Nafasi	3
(vi)	VIJANA - Nafasi	10
Jumla ya nafasi za Wanawake viti maalum katika Bunge		**100**

(3) Kwa upande wa Baraza la Wawakilishi, kutakuwa na jumla ya nafasi 20 za Viti Maalum vya Wanawake. Nafasi 1 (moja) imetengwa na Halmashauri Kuu ya Taifa kwa Kiongozi Mkuu wa UWT Taifa anayetoka Zanzibar. Nafasi 19 zilizobaki zitagombewa na Mikoa yote ya Zanzibar, pamoja na Makundi hayo yaliyotajwa. Nafasi hizo zimegawanywa na Kamati Maalum ya Halmashauri Kuu ya Taifa Zanzibar kama ifuatavyo:-.

(a)	MIKOA MITANO YA ZANZIBAR: Nafasi 2 kwa kila Mkoa kwa Mikoa mitano jumla ya nafasi	10
(b)	MAKUNDI:	
	(i) Vijana - Nafasi	5
	(ii) Wasomi - Nafasi	2
	(iii) Walemavu - Nafasi	2
	(iv) Makamu Mwenyekiti UWT Taifa - Nafasi	1
	Jumla ya nafasi za Wanawake viti maalum katika Baraza la Wawakilishi	**20**

(4) Kamati Kuu ya Halmashauri Kuu ya Taifa itawajadili wagombea wote na kuwatolea mapendekezo yake kwa Halmashauri Kuu ya Taifa; ambayo itafanya uteuzi wa Wagombea na kuwasilisha orodha ya majina yaliyoteuliwa kwa Tume ya Taifa ya Uchaguzi, na kwa Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar.

(5) Tume ya Taifa ya Uchaguzi itatangaza washindi wa Viti Maalum vya Ubunge, na Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar itatangaza washindi wa viti Maalum vya Uwakilishi, kwa kuzingatia masharti ya Katiba ya nchi, na ya Katiba ya Zanzibar.

MALALAMIKO YA UTEUZI WA WAGOMBEA

19 (1) Mara baada ya matokeo ya uteuzi wa mwisho wa wgombea kutangazwa, mwanachama yeyote ambaye hakuteuliwa kugombea nafasi aliyoomba anaweza, endapo anayo malalamiko kuhusu uteuzi huo, kuwasilisha malalamiko yake kwa Katibu wa Chama wa ngazi yenye nafasi aliyoomba. Isipokuwa kwamba kama uteuzi unaolalamikiwa ni wa ngazi ya Taifa, malalamiko yatawasilishwa kwa Katibu Mkuu wa CCM.

(2) Malalalmiko hayo yatawasilishwa kwa maandishi na lazima yaonyeshe kwa ukamilifu mambo yanayolalamikiwa. Jina na anwani ya mlalamikaji lazima vionyeshwe wazi katika barua ya malalamiko.

(3) Malalamiko lazima yawasilishwe ndani ya siku tatu baada ya kutangazwa matokea ya uteuzi, ili kazi ya kuyasikiliza iweze kuanza bila kuchelewa.

(4) Wakati malalamiko yake yanasikilizwa, mgombea mteule anayelalamikiwa ataendelea

KANUNI ZA UTEUZI FEB '10:Layout 1 6/2/10 3:59 PM Page 45

kujiandaa ili asichelewe kuwasilisha fomu zake kwa Msimamizi wa Uchaguzi wa Dola anaohusika.

20. Malalamiko yote ya uteuzi yatamalizwa ndani ya vikao vya Chama haraka iwezekanavyo ili mgombea mteule asichelewe kuwasilisha fomu zake kwa Tume ya Uchaguzi siku ile ya kurudisha fomu (Nomination Day) na kusababisha CCM ikose mgombea kwa sababu tu ya malalamiko hayo.

21. Kwa ngazi za mwanzo, kila Halmashauri Kuu ya CCM ya ngazi ya Katibu aliyepokea malamiko, itakuwa na madaraka ya kuamua malalamiko yote yanayohusu uteuzi. Kwa ngazi ya Taifa, Kamati Kuu itakuwa na madaraka ya kuamua malalamiko yote yanayohusu uteuzi, ambayo Katibu Mkuu wa CCM atakuwa ameyapokea.

MIIKO YA SHUGHULI ZA UCHUJAJI NA UTEUZI WA WAGOMBEA

22. Maadili na nidhamu ya Chama katika kusimamia na kutekeleza shughuli za uteuzi wa wagombea wa CCM katika vyombo vya Dola lazima vizingatiwe na wale wote wanaohusika. Hivyo yawapasa kuelewa na kuzingatia kuwa:-

    (1) Ni mwiko kwa kiongozi yeyote, kwa maneno au vitendo, kumpendelea au kumsaidia kupata kura nyingi mwombaji mmoja dhidi ya mwingine miongoni mwa wale waliorudisha fomu.

KANUNI ZA UTEUZI FEB '10:Layout 1 6/2/10 3:59 PM Page 46

(2) Ni mwiko kabisa kwa mgombea kutumia au kuhusisha ukabila, dini, rushwa, rangi, au eneo analoishi/anakotoka katika shughuli yoyote ya uchaguzi.

(3) Ni mwiko kwa mgombea yeyote kufanya kampeni za kupakana matope, au ya aina nyingine yoyote ile dhidi ya mgombea mwingine.

(4) Ni mwiko kwa kiongozi yeyote au mwombaji yeyote wa nafasi ya uongozi au mwanachama yeyote aliyekabidhiwa dhamana ya usimamizi/uangalizi/uratibu wa kura za maoni, uchujaji na uteuzi, kufanya vitendo vya ukiukaji wa Kanuni hizi, Katiba ya CCM, Sheria, na Kanuni za Uteuzi.

(5) Bila kuathiri haki ya mwanachama yeyote ya kutangaza wakati wowote nia yake ya kutaka kugombea nafasi fulani ya uongozi katika vyombo vya Dola, kwa kuwa nafasi hizo zimewekewa muda maalum wa miaka mitano, itakuwa ni marufuku:-

(a) Kwa mgombea yeyote mtarajiwa au wakala wake, kufanya vitendo vyovyote vinavyoonekana dhahiri kuwa ni sehemu ya kampeni za kuwania nafasi anayoitafuta kabla ya muda rasmi wa uongozi unaohusika haujamalizika.

KANUNI ZA UTEUZI FEB '10:Layout 1 6/2/10 3:59 PM Page 47

(b) Kwa Mgombea yeyote kutoa misaada mbalimbali wakati uchaguzi unapokaribia, ambayo dhahiri ina lengo la kuvutia kura.

Isipokuwa kwamba kanuni hii haitamhusu Rais, Mbunge, Mwakilishi, au Diwani ambaye yupo madarakani wakati huo, kwa kuwa yeye atakuwa bado anao wajibu wa kuhudumia eneo lake la uongozi.

(6) Adhabu za kuvunja miiko iliyotajwa katika Kanuni hii ni hizi zifuatazo:-

(a) Kiongozi yeyote ambaye baada ya kuchaguliwa, atakayethibitika kuvunja miiko hiyo, atavuliwa uongozi wake.

(b) Mwanachama anayeomba kugombea nafasi yoyote atakayethibitika kuvunja miiko hiyo hatateuliwa kugombea nafasi anayoiwania.

KANUNI ZA UTEUZI FEB '10:Layout 1 6/2/10 3:59 PM Page 48

FUNGU LA NNE

MASUALA MUHIMU YA KUZINGATIA WAKATI WA VIKAO VYA UCHUJAJI NA UTEUZI WA WAGOMBEA

23. Ili haki iweze kutendeka wakati wa vikao vya kuchuja au kuteua wagomabea, ni muhimu kuzingatia kwamba:-

    (1) Wajumbe wa Vikao vya uchujaji na uteuzi wa mwisho wa wagombea wasiwe na upendeleo wala ubinafsi katika kutoa uamuzi. Lengo Kuu la uteuzi liwe kumpata mwana-CCM mwenye uwezo mkubwa wa uongozi na anayekubalika na wananchi ili ateuliwe kugombea nafasi ya uongozi iliyopo.

    (2) Wajumbe wa vikao hivyo hawana budi kuepuka kutoa siri za vikao baada ya kukamilisha kazi ya kuwajadili wagombea. Matokeo ya uteuzi wa mwisho yatolewe au yatangazwe kwa kuzingatia utaratibu uliowekwa. Mjumbe atakayevunja kifungu hiki cha Kanuni atadhibitiwa na Kamati ya usalama na maadili ya ngazi inayohusika.

    (3) Wajumbe wa Vikao vya uchujaji na uteuzi wa Wagombea kwa ngazi inayohusika hawaruhusiwi kuendelea na kazi ya uchujaji na uteuzi iwapo wao ni wagombea katika ngazi

KANUNI ZA UTEUZI FEB '10:Layout 1 6/2/10 3:59 PM Page 49

hiyo. Akidi ya wajumbe ikipungua, na kwa kuwa hili litakuwa limefahamika mapema kabla ya kikao, Halmashauri Kuu ya ngazi hiyo iteuwe wajumbe wengine kutoka miongoni mwao wa kukamilisha Akidi. Idadi ya watakaoteuliwa ilingane na ya wajumbe waliozuiwa kushiriki kwa kuwa ni wagombea.

(4) Wajumbe wa Vikao vya uteuzi wazingatie kwa makini nidhamu na maadili ya vikao vya CCM.

“Inawezekana, timiza wajibu wako”
(Baba wa Taifa, Mwl. J.K. Nyerere)

KANUNI ZA UTEUZI FEB '10:Layout 1 6/2/10 3:59 PM Page 50

KANUNI ZA UTEUZI FEB '10:Layout 1 6/2/10 3:59 PM Page 51

KANUNI ZA UTEUZI FEB '10:Layout 1 6/2/10 3:59 PM Page 52